

2022

# TCCIA INVESTMENT PLC
## MKUTANO MKUU WA 17 WA WANAHISA 05/11/2022



# TAARIFA YA KAMPUNI

Kwenye Mkutano Mkuu wa 17 wa Wanahisa

## TAARIFA YA KUITISHA MKUTANO NA AKIDI

Wanahisa wanaombwa kuzingatia taarifa iliyotolewa kulingana na kifungu Namba 33 cha Kanuni za Kampuni kinachohusu uitishaji wa Mkutano Mkuu wa Wanahisa.

Wanahisa wanaombwa kuzingatia kuwa, akidi kwa mujibu wa kifungu Na. 38 cha Kanuni za Kampuni ni idadi ya wanahisa wasiopungua 10 wanaomiliki hisa zaidi ya asilimia 50.



### TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA

UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 05 Novemba, 2022.
Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa kumi na saba wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 05 Novemba, 2022 kwa njia ya mtandao.

# KUPOKEA AJENDA

Wanahisa mnaombwa kupokea Ajenda kama zilivyowasilishwa.



Dondoo Na. 17/2/2022

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 05 NOVEMBA, 2022.

Tunapenda kukujulisha kuwa, Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 05 Novemba, 2022 kwa njia ya mtandao. Mkutano utaanza saa Tatu kamili (3:00) asubuhi. Kampuni itawatumia Wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidigitali.

**Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba ni:**

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba;
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba;
3. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita;
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita;
5. Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021;
6. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2021;
7. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2022;
8. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi;
9. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Kampuni kununua baadhi ya hisa zake (share buy back);
10. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la kuorodheshwa hisa za Kampuni kwenye soko la hisa la Afrinex-Mauritius (Cross-Listing);
11. Kupokea, kujadili na kuamua mapendekezo kutoka kwa Wanahisa;
12. Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba.

**Maelezo:**

1. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 11 yatumwe na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 25/10/2022;
2. Taarifa ya Mwaka 2021 na Makabrasha ya Mkutano itapatikana kwenye tovuti ya Kampuni *(https://www.tcciainvest.co.tz)* kuanzia tarehe 25/10/2022;
3. Endapo Mwanahisa atashindwa kuhudhuria anaombwa, kuteua Mwakilishi atakayehudhuria Mkutano kwa niaba yake. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni *(https:// www.tcciainvest.co.tz)*. Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe *info@tcciainvest.co.tz* au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na. 0757-138048 na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 03/11/2022. saa kumi kamili jioni.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

**Peter W. Kifunguomali**
Katibu
Tarehe: **20/09/2022**

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA WA WANAHISA ULIOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI, TAREHE 20 NOVEMBA, 2021 KWA NJIA YA MTANDAO.

## 16.1 WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| Bw. Fortunatus Magambo | - | Mwenyekiti |
| Bw. Peter W. Kifunguomali | - | Katibu |

Orodha ya Wajumbe pamoja na Wawakilishi wa Wanahisa waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita uliofanyika siku ya Jumamosi tarehe 20 Novemba, 2021 imeambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi. Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1.

## 16.2 KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA

Mwenyekiti alifungua Mkutano kwa kuwakaribisha Wanahisa, Wajumbe wa Bodi, Wageni Waalikwa na Wafanyakazi wa Kampuni kwenye Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka. Baada ya Kutolewa taarifa kwamba Akidi ilikuwa imetimia kulingana na Kifungu Namba 38 cha Kanuni za Kampuni, Mwenyekiti alifungua Mkutano saa 3:05 Asubuhi.

## 16.3 KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA

Hakukuwa na Mabadiliko yoyote hivyo, Wajumbe walipitisha Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita kama zilivyosomwa na Katibu wa Bodi.

## 16.4 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO

Wajumbe walithibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano na zikasainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

## 16.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO ULIOFANYIKA TAREHE 10 AGOSTI, 2020

Taarifa ilitolewa kuhusu utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyopitishwa na Wajumbe wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano uliofanyika tarehe 20 Agosti, 2020 na kukubaliwa na Wanahisa.

## 16.6 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2020

16.6.1 Taarifa ya Wakurugenzi iliwasilishwa na kukubaliana na wajumbe na kushauri;

16.6.1.2 Ni vema Bodi iendelee kuangalia namna ya kuongeza mapato ya Kampuni na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima;

16.6.1.3 Kuangalia fursa mbalimbali katika uwekezaji katika sekta ya viwanda;

16.6.1.4 Pia inaendelea kuangalia maeneo mengine yenye tija zaidi;

16.6.1.5 Mwenyekiti aliwajulisha wajumbe kuwa, Kampuni imeshachukua hatua ya kuwekeza katika Amana za Serikali.

## 16.7 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA MAHESABU YA KAMPUNI YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2020

Taarifa ya Mahesabu iliwasilishwa na haikukinzana na taarifa nyingine. Kulingana na Taarifa ya mahesabu, shughuli za Kampuni zitaendelea bila kuathiriwa na chochote. Mkaguzi wa Mahesabu aliwajulisha wajumbe kuwa, kwa mwaka wa fedha wa 2020, Kampuni Ilipata Hati safi. Iliazimiwa kwamba, Taarifa ya mahesabu ya Kampuni yaliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2020 yamepitishwa kama yalivyowasilishwa.

## 16.8 AZIMIO KUHUSU MALIPO YA GAWIO

Taarifa ilitolewa kuwa, azimio hili limetekelezwa kwa kuwalipa Wanahisa ambao taarifa zao katika Daftari la Wanahisa zilikuwa zimerekebishwa. Kila Mwanahisa alilipwa gawio la shilingi 6 kwa kila hisa moja.

## 16.9 KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA BODI KUHUSU MALIPO YA GAWIO KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2020

Bodi ilipendekeza kuwa malipo, ya gawio kwa wanahisa yafanyike siku tisini (90) baada ya kupitisha azimio.

Kwa Wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

Mkutano Mkuu uliazimia na kuridhia gawio la shilingi sita za Kitanzania (6) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.

## 16.10 UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2021

Bodi ilipendekeza kuwa, CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2021. Ada ya Ukaguzi iliyopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 20 milioni kabla ya kodi. Ilielezwa kuwa ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

Iliazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2021. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 20 milioni kabla ya VAT kama gharama za malipo ya ukaguzi wa mahesabu ya Kampuni.

## 16.11 PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Mkutano Mkuu uliarifiwa kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, 2021. Menejimenti ilipendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000), kwa kuwa kiasi hiki kimezingatia mazingira ya sasa na pia Wakurugenzi walilkuwa wakilipwa kiasi cha shilingi milioni nne kwa kipindi cha miaka minne. Iliazimiwa kwamba, kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi.

## 16.12 KUPOKEA, NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MABADILIKO KWENYE DAFTARI LA WANAHISA

Mkutano Mkuu uliarifiwa kuwa, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ilielekeza bodi kurekebisha kasoro kwenye daftari la Wanahisa. Kulingana na taarifa sahihi ya idadi za hisa zinazoonyeshwa kwenye taarifa ya hesabu za Kampuni ni 72,957,660, tofauti na taarifa zilizopo kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ambazo ni 73,077,253, hii ikiwa ni tofauti ya hisa 119,593.

Mkutano Mkuu uliridhia kurekebisha kasoro zilizojitokeza kwa kuondoa tofauti ya hisa 119,593 kati ya taarifa zilizopo kwenye hesabu za Kampuni na taarifa zilizopo kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.

## 16.13 UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BODI

Mkutano Mkuu uliarifiwa kwamba, Kifungu Namba 69 cha Katiba ya Kampuni, kinatamka kuwa idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi itakuwa si chini ya 5 wala haitazidi 7 kama ifuatavyo.

**16.13.1** Kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma utengewe nafasi mbili kwa kuwa PSSSF inamiliki asilimia 38.52 ya hisa za Kampuni. Mfuko uliwateua Bwana Fortunatus Magambo na Bwana Ernest R. Khisombi.

**16.13.2** Chemba ya Wafanya Biashara, Wenye Viwanda na Kilimo itengewe nafasi moja ambayo Mjumbe atakuwa ni Rais wa Chemba akiwakilisha Wanahisa wadogo ambao wengi ni wanachama wa Chemba. Chemba inawakilishwa na Bwana. Paul F. Koyi.

**16.13.3** Mjumbe mmoja achaguliwe kutoka Kundi la Wanataaluma. Mjumbe huyo atapigiwa kura na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu. Mkutano Mkuu ulimchagua Bwana Nathan E. Mnyawami kutoka kundi la wataalam.

**16.13.4** Wajumbe ambao ni Wanahisa wenye sifa stahiki.

Wajumbe wengine ambao ni wanahisa waliochaguliwa kulingana na sifa zilizoainishwa ni kama ifuatavyo: -

**Prof. Lucian A. Msambichaka**
**Ndugu. Joseph M. Kahungwa**
**Bi. Magdalene N. E. Mkocha**

## 16.14 KUFUNGA KWA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA

Mwenyekiti wa Bodi aliwashukuru wanahisa wote, Wajumbe wa Bodi, Wafanyakazi pamoja na wageni waalikwa wote kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa 16 pamoja na mchango wao katika kuboresha maendeleo ya Kampuni.

Mkutano ulifungwa saa 4:13 Asubuhi

| | |
|---|---|
| ............................................................ | ............................................................ |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| Tarehe: | Tarehe: |

## KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA WA MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 20 NOVEMBA, 2021

**WASILISHO**

Wanahisa wanaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 16 uliofanyika tarehe 20, Novemba, 2021 kama kumbukumbu sahihi:-

### "Azimio la 1/2022

Imeazimiwa kuwa Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa kumi na Sita ulifanyika tarehe 20 Novemba, 2021 ni kumbukumbu sahihi"

## YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU ULIOPITA

*Jedwali na. 1*

| Kumb | Maelezo mafupi | Azimio | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| **16.9** | Malipo ya Gawio | Gawio lilipwe Shilingi sita (6) kwa kila hisa moja. | Limetekelezwa kwa wale ambao taarifa zao zimekamilika. |
| **16.10** | Kuteua Mkaguzi wa Mahesabu | Mkutano Mkuu uliidhinisha CROWE Tanzania kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021 | Limetekelezwa. |
| **16.11** | Malipo ya Wakurugenzi | Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi 4,800,000 kwa kila mjumbe kwa mwaka 2020. | Limetekelezwa. |
| **16.12** | Mabadiliko Kwenye daftari la wanahisa | Kuondoa tofauti ya Hisa 119,593 kati ya taarifa zilizopo kwenye hesabu za Kampuni na taarifa zilizopo Soko la Hisa Dar es Salaam | Agizo hili limetekelezwa na kusajiliwa BRELA |



Dondoo Na. 17/5/2022

# KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI NA TAARIFA YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2021.

Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa iko katika Taarifa ya Mwaka.

# TAARIFA YA MWENYEKITI

*"Tunahitaji kuhakikisha Kampuni inakua pamoja na kuimarisha mifumo ya utendaji na kuwa na biashara endelevu. Hatua kwa hatua, tunaweza kugeuza maono ya kampuni na kutengezeza faida zaidi kwa wanahisa."*

Fortunatus M. Magambo



## UTANGULIZI

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninayo furaha kuwasilisha taarifa ya utendaji kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2021. Licha ya changamoto mbalimbali, bado Kampuni imeendelea kufanya vizuri. Taarifa ya utendaji inaonyesha ongezeko la mapato ya Kampuni lakini pia Bodi na Menejimenti inaendelea kuchukua hatua madhubuti kuendelea kukuza ongezeko la thamani kwa wanahisa wake.

## BIASHARA ENDELEVU

Biashara endelevu ni jambo la msingi katika kuboresha ukuaji wa uchumi wa Kampuni na wa muda mrefu. Hata hivyo, tuna imani ya kuendelea kufanya vizuri katika utendaji na kutimiza malengo ambayo Kampuni imejiwekea. Uimara wa Kampuni ni nguzo muhimu katika utendaji. Ili Kampuni kuendelea na shughuli zake za kibiashara tunaamini kuwa kufanya kazi pamoja kwa kushirikiana na wadau wetu wakuu kunaweza kuleta ufanisi zaidi na mazingira salama ya kiutendaji.

Tunahitaji kuhakikisha Kampuni inakua, pamoja na kuimarisha mifumo ya utendaji na kuwa na biashara endelevu. Hatua kwa hatua, tunaweza kugeuza maono ya Kampuni na kutengezeza faida zaidi kwa wanahisa.

## GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2021, Bodi inapendekeza malipo ya gawio yawe Shilingi 10 kwa hisa. Malipo ya gawio yaliyopendekezwa yanategemewa kuidhinishwa na wanahisa wakati wa Mkutano Mkuu huu wa 17.

## MATARAJIO YA BAADAYE

Kwa mwaka 2022, Bodi itajikita katika utekelezaji wa mipango iliyowekwa ya kukuza vyanzo vya mapato na kuongeza ufanisi wa kazi. Tunatarajia kuigeuza TICL kuwa chombo chenye mafanikio kwa kuwekeza katika fursa mbalimbali zinazojitokeza ndani na nje ya nchi.

## SHUKRANI

Natoa shukurani kwa Wakurugenzi wenzangu katika Bodi ya Wakurugenzi iliyoundwa upya. Wametoa fursa ya ushauri wa kusimamia Kampuni yetu. Nawashukuru sana Wanahisa wetu, wateja na washirika wa biashara wanastahili shukrani zangu za kina kwa msaada wao ulioifanya Kampuni yetu kukua. Mwisho, siwezi kusahau shukrani kwa CMSA (Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana), DSE (Soko la Hisa la Dar es Salaam) na wakala wengine wa udhibiti kwa mwongozo na usimamizi wao. Mwisho kabisa, Uongozi wa Kampuni unastahili kupongezwa kwa ari na maono yake mapana katika kutekeleza malengo ya kimkakati yaliyowekwa ya kuisukuma TICL na kuifanya ipite katika mazingira ya leo yenye misukosuko ya biashara ambapo ushindani ni mkali.

Ahsante sana.

......................................

**Fortunatus M. Magambo**
Mwenyekiti wa Bodi
Tarehe: **30/05/2022**

## TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU

*"Mwanga umeanza kuonekana katika wingu zito lililokuwa limetanda kwenye ukuaji wa Kampuni wa sasa na matarajio ya siku zijazo yameanza kuonekana.."*

Peter W. Kifunguomali



### UTANGULIZI

Kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2021, tumepiga hatua mbalimbali katika mwaka wa pili wa kutekeleza Mpango Mkakati wa Kampuni wa miaka mitatu 2020 - 2022. Mpango wetu ni kuongeza faida, Kuongeza fedha kwenye mzunguko na kuongeza mapato ya Kampuni. Lengo kuu ni kubadili mfumo wa sasa na wa baadaye kwa kuwekeza ndani na nje ya nchi. Tunafanya jitihada kuimarisha ongezeko la thamani kwa Wanahisa, kuwekeza na kuboresha utendaji. Bodi na Menejimenti wanajitoa kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha lengo la Kampuni linatimia.

Mwanga umeanza kuonekana kwenye ukuaji wa Kampuni wa sasa na matarajio ya siku zijazo yameanza kuonekana.

### MAPATO KATIKA UWEKEZAJI

Kampuni imepanua wigo wake kwa kusimamia vizuri uwekezaji ambapo kwa asilimia kubwa imewekeza kwenye hisa na dhamana za serikali kutoka TZS 2,000,000 mwaka 2005 na kufikia TZS 29,397,763,000 mwaka 2021. Mapato ya Kampuni yameongezeka kutoka asilimia nane (8%) na kufikia asilimia kumi na tano (15%). Hivyo, Kampuni imeendelea kutoa Gawio kwa wanahisa wake mfululizo kutoka mwaka 2012.

### TAARIFA YA KIUTENDAJI

Kampuni imeendelea kufanya vizuri. Mapato pamoja na uwekezaji vimeongezeka kwa mwaka 2021 ukilinganisha na taarifa ya mwaka 2020 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

*Jedwali na. 2*

| MAELEZO | MAELEZO | 2021 | 2020 |
|---|---|---|---|
| Mapato | Shilingi'000 | 2,690,726 | 2,507,571 |
| Gharama za Uendeshaji wa Kampuni | Shilingi'000 | (1,014,150) | (1,060,243) |
| Faida baada ya Kukata Kodi | Shilingi'000 | 1,329,859 | (475,136) |
| Mali za Wanahisa | Shilingi'000 | 27,404,314 | 26,571,009 |
| Jumla ya mali za Kampuni | Shilingi'000 | 30,451,345 | 29,777,019 |
| Pato kwa kila Hisa (EPS) Earnings per shares | Shilingi'000 | 18.22 | (6.51) |

## Taarifa ya Afisa Mtendaji Mkuu...

**UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI**

Kwa mwaka 2021, kazi kubwa iliyofanywa na Kampuni ni kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Kampuni iliwekeza jumla ya Shilingi 4,597,335,000 kwenye Amana za Serikali (Government Bonds) za miaka 25 na Shilingi 1,048,815,000 kwa kununua hisa baada ya kuuza Amana za Serikali na baadhi ya hisa tulizowekeza kwenye Makampuni mengine kama njia mojawapo ya kutanua wigo wa uwekezaji.

Hadi kufikia Desemba 31, 2021, Uwekezaji uliongezeka kwa asilimia mbili (2%) na kufikia Shilingi 29,397,763,000 ukilinganisha na Shilingi 28,817,636,000 mwaka 2020.

Maeneo ambayo Kampuni iliwekeza kufikia Desemba 31, 2021 kwa muhtasari ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

*Jedwali na. 3*

| AINA YA UWEKEZAJI | 2021 (SHS'000') | % | 2020 (SHS'000') | % |
|---|---|---|---|---|
| Hisa | 15,253,840 | 52 | 14,848,114 | 52 |
| Amana za Serikali | 12,985,104 | 44 | 13,578,175 | 47 |
| Amana za Benki | 932,472 | 3 | 155,000 | - |
| Amana za Makampuni | - | - | 10,000 | - |
| Mali zisizohamishika | 221,347 | 1 | 221,347 | 1 |
| Maeneo mengine | 5,000 | - | | - |
| Jumla ya Uwekezaji | 29,397,763 | 100 | 28,817,636 | 100 |

**MTAZAMO WA BIASHARA**

Kwa kuzingatia siku zijazo, tuna uhakika kwamba mazingira yetu ya uwekezaji yanafaa kwa kuanzisha miradi muhimu kama vile kilimo na biashara ya mifugo ambayo ina uhusiano wa moja kwa moja na wananchi. Aidha, ushiriki wetu katika sekta ya uzalishaji ni kuthamini mwenendo wa uchumi wa nchi. Tutategemea pia kupunguza uwekezaji kwenye hisa ili kupunguza uwezekano wa athari zinazoweza kujitokeza na kuathiri mwenendo wa Kampuni.

**HITIMISHO**

Tuna wafanyakazi bora na waliojitolea kuwa familia ya TCCIA Investment PLC ambao wanaelewa malengo ya kimkakati ya Kampuni vizuri; ni wanaume na wanawake wenye sifa na utendaji bora.

Ninaishukuru sana Bodi ya Wakurugenzi kwa mwongozo mzuri, Menejimenti, mabenki, wakaguzi, na wawekezaji kwa nia yao kubwa ya kuhakikisha kwamba Kampuni yetu inafanikiwa kwa kila inachofanya katika kukua kwake.

Ahsanteni sana

......................................

**Peter William Kifunguomali**
Afisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: **30/05/2022**

# TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 Desemba, 2021

## UTANGULIZI

Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Wakurugenzi pamoja na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021. Taarifa hii inatoa picha kamili ya hali halisi ya Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2021.

## UANZISHWAJI WA KAMPUNI

Kampuni ilianzishwa Tanzania kulingana na Sheria za Makampuni ya mwaka 2002. Kampuni imesajiliwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam na inamilikiwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## BIASHARA YA KAMPUNI

Biashara kuu ya Kampuni ni uwekezaji katika hisa za Makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na Amana za Makampuni ambazo zinatoa faida kubwa na Amana za Serikali pamoja na uwekezaji katika maghala ambayo yako maeneo yenye mpango mkakati mzuri.

Aidha, Kampuni inahimiza kujenga utamaduni wa kuweka akiba kwa wanahisa wake kwa njia ya kuwekeza katika hisa za makampuni yenye ufanisi mkubwa.

## MAONO, DHIMA, KAULI MBIU NA MAADILI KATIKA KAZI

**DHIMA YA KAMPUNI**
Kutengeneza ongezeko la thamani ya muda mrefu kwa wanahisa wa Kampuni kwa kutoa faida nzuri zaidi inayotokana na uwekezaji bora na salama.

**MAONO YA KAMPUNI**
Kuwa kituo kikuu cha usimamizi wa uwekezaji Tanzania.

**KAULI MBIU**
Kwa pamoja tunaweza.

**MAADILI KATIKA KAZI:**
Uwajibikaji, Kujitoa, Kufanya kazi kwa pamoja, Uaminifu na uvumbuzi.

## MATOKEO YA SHUGHULI ZA BIASHARA

Taarifa za Mahesabu zinaandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Taarifa za Mahesabu (IFRS) na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Sera za uhasibu zimetumika ipasavyo ikilinganishwa na mwaka jana, isipokuwa kwa kupitishwa kwa Sheria mpya ya Uandaaji wa Taarifa za Mahesabu au zilizorekebishwa kama ilivyoainishwa katika kidokezo namba moja.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021, Kampuni ilipata faida ya Shilingi 1,329,860,000 baada ya kodi ikilinganishwa na hasara ya TZS Shilingi 475,136,000 mwaka 2020 baada ya kodi. Mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa asilimia saba (7%) kutoka Shilingi 2,507,571,000 mwaka 2020 na kufikia Shilingi 2,690,726,000 mwaka 2021. Kuongezeka kwa mapato kunatokana na uamuzi wa Bodi wa kubadilisha mfumo wa uwekezaji wa Kampuni na kuwekeza zaidi katika Amana za Serikali na kwenye hisa.

## IDADI YA HISA ZA KAMPUNI

*Jedwali na. 4*

| | | | IDADI YA HISA | |
|---|---|---|---|---|
| Zilizoidhinishwa (Authorized) | | | **2021** | **2020** |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | | | 5,000,000,000 | 5,000,000,000 |
| | | | | |
| | **2021** | **2020** | **2021** | **2020** |
| | Shs'000 | Shs'000 | **Idadi ya Hisa** | |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | 1,459,153 | 1,459,153 | 72,957,660 | 72,957,660 |
| Share Premium | 708,799 | 708,799 | - | - |
| | 2,167,952 | 2,167,952 | 72,957,660 | 72,957,660 |

Hapakuwa na mabadiliko yoyote ya idadi ya hisa zinazomilikiwa na Kampuni kwa mwaka 2021.

## GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2021, Bodi inapendekeza gawio la Shilingi 10 kwa kila hisa moja ambayo ni sawa na Shilingi 729,576,600 ukilinganisha na gawio la Shilingi 6 kwa kila hisa moja sawa na Shilingi 438,463,518 mwaka 2020.

## DHUMUNI NA MPANGO MKAKATI WA KAMPUNI

**Ongezeko la Thamani**: Kuiwezesha Kampuni kufikia lengo la wanahisa la kuanzishwa kwa hii Kampuni. Lengo kuu ni kuongeza thamani ya Hisa na kukuza mtaji wa Kampuni. Kampuni pia inalenga kuanzisha Kampuni tanzu ili kugawanya mtaji wake katika maeneo mengine ya biashara.

**Uwekezaji Bora:** Kampuni ina lengo la kuimarisha thamani ya Kampuni kwa kuimarisha rasilimali za Kampuni na kuongeza kipato katika uwekezaji. Kampuni ina mpango wa kukuza kipato kupitia uwekezaji kwa asilimia ishirini na mbili (22%) kwa mwaka.

**Utendaji Bora:** Kampuni ina mpango wa kuimarisha utendaji kupitia wafanyakazi waliopo na teknolojia ili kukuza ufanisi, kuhudumia wanahisa, kukidhi matakwa ya mamlaka zinazoisimamia, kuimarisha utamaduni wa ushirikiano, kuimarisha maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha utendaji na uwajibikaji wa wafanyakazi. Pia, Kampuni ina mpango wa kufanikisha mipango yake kwa asilimia tisini na tano (95%).

## WAKURUGENZI WA KAMPUNI

Kwa mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2021, Wakurugenzi walikuwa ni hawa wafuatao:-

*Jedwali na. 5*

| NAME | NAFASI | URAIA | SIFA/ELIMU |
|---|---|---|---|
| Bwn. Fortunatus Magambo | Mwenyekiti | Mtanzania | Mchumi |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | Mtanzania | Mchumi |
| Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | Mtanzania | Mhasibu |
| Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | Mtanzania | Kilimo/Mchumi |
| Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | Mtanzania | Mchumi |
| Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | Mtanzania | Mauzo na Manunuzi |
| Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe | Mtanzania | Teknohama |

Hapakuwa na mabadiliko yoyote ya Wakurugenzi kwa mwaka 2021.

## MATUKIO BAADA YA TAARIFA HII

Hapakuwa na tukio lolote lililojitokeza baada ya kutolewa kwa taarifa hii.

## KATIBU WA BODI

Kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2021, hapakuwa na mabadiliko yoyote ya Katibu, bali ameendelea kuwa Ndugu Peter William Kifunguomali.

## SIASA NA KUSAIDIA JAMII

Kulingana na Sera ya Kampuni, hatujawahi kuchangia shughuli za siasa.
Hata hivyo, kwa kutambua umuhimu wa elimu katika jamii yetu, kwa mwaka 2021 Kampuni imechangia Shilingi milioni mbili kwa shule ya Sekondari Mkomazi kwa ajili ya kununua madawati ukilinganisha na Shilingi milioni tano ambazo zilitolewa mwaka 2020.

## UDHIBITI WA ATHARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA NA MFUMO WA NDANI

Bodi ina wajibu wa kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza pamoja na kusimamia mfumo mzima wa utendaji kwenye Kampuni. Menejimenti inawajibika kuhakikisha taarifa ya Mahesabu na Mfumo wa Utendaji unafanya vizuri. Lengo ni kuhakikisha ufanisi katika mfumo wa utendaji kama ifuatavyo:

- Kulinda stahiki za wanahisa na mali za Kampuni.
- Ufanisi na Ubora katika kazi;
- Kukidhi matakwa ya Mamlaka na Sheria.
- Kuwepo kwa rekodi ya Mahesabu na Taarifa ya Fedha.
- Kampuni kuendelea na shughuli za utendaji katika mazingira ya kawaida na yasiyo ya kawaida.
- Kuwajibika kwa wadau wa Kampuni.

Ufanisi na udhibiti wa mfumo wowote wa utendaji wa ndani unategemea utaratibu na hatua zilizochukuliwa. Kuna athari zinazoweza kujitokeza kwa kushindwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa wafanyakazi. Hakuna mfumo wa udhibiti wa ndani unaoweza kutoa taarifa kamili dhidi ya taarifa potofu au hasara kwa sababu mfumo wa Kampuni umeundwa kuwapa Wakurugenzi uhakika kwamba taratibu zilizopo zinafanya kazi kwa ufanisi. Wakurugenzi wamethibitisha mfumo wa ndani wa utendaji na kujiridhisha kuwa unafanya kazi vizuri.

Kampuni ina sera mbalimbali ambapo kupitia hizo inaweza kudhibiti athari kwenye Kampuni. Na kwa upande mwingine, Kampuni imemwajiri Mkaguzi wa ndani wa muda, ambaye anasimamiwa na Bodi kupitia Kamati ya Ukaguzi ambapo kupitia yeye Bodi inaweza kusimamia utendaji wa Kampuni kwa ufanisi mkubwa.

### Tathmini na Athari za Kampuni na Namna ya Kuzizuia.

Kampuni imewekeza katika taasisi za fedha ikiwemo Amana za serikali za muda mfupi na muda mrefu, Amana za Makampuni, mikopo, amana za mabenki na kwenye hisa. Maeneo mengine ya uwekezaji ni pamoja na biashara zinazotoa faida. Lengo la uwekezaji huu ni kuongeza mapato kwenye Kampuni.

Athari zinazoweza kuikumba Kampuni ni pamoja na: -

### Athari za Kutopata Faida

Athari ya kutopata faida ni athari ya soko inayotokana na mabadiliko ya thamani ya mali ya Kampuni kama matokeo ya kushuka kwa bei katika uwekezaji wa Kampuni. Uwekezaji katika amana za serikali za muda mrefu na mapato ya kudumu ni njia mojawapo ya kupunguza athari ya kushuka kwa viwango vya riba katika soko.

### Athari ya Hisa Kushindwa Kuuzwa

Hii athari inatokana na kushindwa kufikia malengo. Lakini pia hii athari inatokana na kushindwa kuuza hisa kwa wakati na kwa bei iliyokusudiwa. Kampuni inaweza kupunguza hii athari kwa kuwekeza kwenye amana za benki za muda mfupi zinazoweza kukamilisha mipango yake ya uwekezaji na matumizi ya ndani ya Kampuni.

Kampuni imekuwa ikifanya makisio ya mapato na matumizi ya kila mwezi. Kampuni inategemea kipato chake kikubwa toka kwenye Magawio kutoka kwenye Makampuni inayomiliki hisa na maeneo mengine ilikowekeza.

**Athari za Mikopo**

Hii inatokana na upande mmoja kushindwa kutimiza wajibu wake wa kulipa deni kwa tarehe iliyopangwa. Ili kupunguza hii athari, Kampuni imeandaa sera ya uwekezaji, kutathmini kabla ya kufanya uwekezaji na ngazi za uidhinishaji katika kila eneo la uwekezaji.

**Athari za Kiutendaji**

Hii inatokana na mfumo duni, usimamizi dhaifu, utendaji dhaifu, udanganyifu katika kazi, wizi na makosa mengine ya kibinadamu. Kampuni inajitahidi kuiepuka hii athari kwa kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa ndani wa Kampuni. Moja ya mbinu za kudhibiti ni pamoja na kufuata miongozo ya kiutendaji na taratibu zilizowekwa, sera na miongozo na kuajiri Mkaguzi wa ndani wa muda. Kusimamia athari za kiutendaji katika Kampuni ni muhimu katika shughuli za kila siku. Kamati ya usimamizi, Mkaguzi wa Ndani wa muda, Kamati ya Ukaguzi na Bodi ya Wakurugenzi wanahusika kikamilifu katika usimamizi wa Kampuni.

**Athari za Rasilimali Watu**

Kulingana na uhalisia wa shughuli za Kampuni, inahitaji wafanyakazi wenye nidhamu na wenye maarifa maalum katika maeneo muhimu ya kiutendaji. Muundo wa Wafanyakazi wa Kampuni unaisaidia Kampuni kuingiza mapato makubwa. Ili kuhakikisha athari hii ya rasilimali watu inazuiwa, Kampuni inahakikisha inawekeza kwa wafanyakazi wake, kupitia kuboresha maslahi yao kila mara.

**Athari ya Kampuni Kupoteza Sifa yake Nzuri**

Kampuni ina wajibu wa kuhakikisha majukumu yake yanafanyika vizuri ili kulinda sifa yake katika makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa kulingana na sheria na taratibu husika. Katika kuhakikisha hili linafanyika, Bodi na Menejimenti zinahakikisha zinatimiza wajibu wake kwa kuzingatia sheria za utawala bora.

**Idadi ya Hisa zinazomilikiwa na Wajumbe wa Bodi kwenye Kampuni**

Mpaka kufikia Desemba 31, 2021, idadi ya Hisa za kila Mjumbe wa Bodi ni kama ifuatavyo:

*Jedwali na. 6*

| WAKURUGENZI | IDADI YA HISA ANAZOMILIKI | |
|---|---|---|
| | **2021** | **2020** |
| Prof. Lucian Ambrose Msambichaka | 487,580 | 487,580 |
| Bwn. Joseph Matanga Kahungwa | 40,600 | 40,600 |
| Bwn. Nathan Edward Mnyawami | 19,675 | 19,675 |
| Bi. Magdalene Nelson Enock Mkocha | 102,363 | 102,363 |
| | **650,218** | **650,218** |

- Bwn. Paul F. Koyi, Rais wa TCCIA - Anawakilisha TCCIA Makao Makuu na Ofisi za Matawi yake zilizoko Mikoa yote ya Tanzania ambao wanamiliki jumla ya Hisa 830,213.
- Bwn. Fortunatus Magambo and Bwn. Ernest R. Khisombi kwa pamoja wanawakilisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali (PSSSF) unaomiliki jumla ya Hisa 28,100,300.


Hakuna mabadiliko yaliyojitokeza kati ya kipindi cha uandaaji wa taarifa hii hadi leo inapowasilishwa.

## UTAWALA BORA

Bodi inawajibika kwa shughuli zote za Kampuni. Pamoja na mambo mengine, Bodi ina wajibu wa kutambua athari ambazo zinaweza kuathiri shughuli za Kampuni, kutafuta fursa na kufanya maamuzi yahusuyo uwekezaji. Bodi ina wajibu wa kuhakikisha mfumo wa utendaji unadhibitiwa ipatasavyo pamoja na sera zote zinatumika na mfumo wa Utawala bora unafuatwa pamoja na taratibu zote.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2021, Bodi ilikutana mara saba (7), ambapo Vikao vya kawaida vilikuwa nne (4) na vikao maalum tatu (3) ambavyo vilifanyika kuidhinisha mambo muhimu ambayo yalikuwa yanahitaji idhini ya Bodi. Bodi imekabidhi usimamizi wa shughuli za kila siku za Kampuni kwa Afisa Mtendaji Mkuu akisaidiwa na Menejimenti. Menejimenti pia inaalikwa kuhudhuria vikao vya Bodi ili kuimarisha ufanisi katika shughuli za Kampuni na Utawala bora. Lengo la kufanyika kwa vikao maalum, ni pamoja ya kujadili na kuidhinisha Mpango Mkakati wa Kampuni na Bajeti ya mwaka pamoja na kupitia Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa.

### WAJUMBE WA BODI PAMOJA NA IDADI YA VIKAO WALIVYOHUDHURIA KWA MWAKA 2021.




*Jedwali na. 7*

| NA. | JINA | NAFASI | IDADI YA VIKAO | IDADI YA VIKAO ALIVYOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bwn. Fortunatus Magambo | Mwenyekiti | 7 | 7 |
| 2. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | 7 | 7 |
| 3. | Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 7 | 7 |
| 4. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 7 | 7 |
| 5. | Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 7 | 7 |
| 7. | Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe | 7 | 6 |
| 8. | Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 7 | 7 |

Wakurugenzi wote wana sifa na uzoefu unaojitegemea ambao unasaidia katika kufanya maamuzi. Wakurugenzi wote wana tabia njema na wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu.
Wakurugenzi wote wanafuata kanuni za Utawala Bora. Kwa mwaka wa fedha wa 2021, Bodi iliunda Kamati mbili ili kutimiza kanuni za Utawala Bora na kufanya maamuzi kwa wakati sahihi kuhusiana na mambo ya Kampuni. Kamati hizo ni:-

- Kamati ya Uwekezaji ambayo ina wajumbe watatu.
- Kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ambayo ina wajumbe watatu.

*Jedwali na. 8*

| | Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji: | |
|---|---|---|
| 1. | Prof. Lucian A. Msambichaka | **Mwenyekiti** |
| 2. | Bwn. Nathan E. Mnyawami | **Mjumbe** |
| 3. | Bwn. Paul F. Koyi | **Mjumbe** |

Kamati ya Uwekezaji ilikutana mara nne (4) kujadili taarifa ya Kampuni ya kila robo mwaka, na Mpango Mkakati wa mwaka pamoja na Bajeti ya Kampuni kabla ya kuwasilisha kwenye Bodi kwa majadiliano na kuidhinisha.

### WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA KUZUIA ATHARI KATIKA KAMPUNI: -

*Jedwali na. 9*

| | WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA KUZUIA ATHARI KATIKA KAMPUNI: | |
|---|---|---|
| 1. | Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mwenyekiti |
| 2. | Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe |
| 3. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe |

Kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ilikutana mara saba (7) kujadili Taarifa ya Kampuni inayoandaliwa na Mkaguzi wa ndani na pia kupitia mahesabu ya Kampuni ya Mwaka mzima.

### MAJUKUMU YA BODI KWA MWAKA 2021

Pamoja na Kusimamia shughuli za Bodi kwa mwaka 2021, Bodi ina majukumu yafuatayo:-

- Kuhakiki Taarifa za wanahisa wa Kampuni;
- Kupitia taarifa ya Kampuni iliyoandaliwa na Mkaguzi wa ndani;
- Kutafuta njia mbalimbali za kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni na kuongeza mapato;
- Kuandaa mpango mkakati na kupitisha bajeti ya mwaka 2022;
- Kufanya Upembuzi yakinifu na kutafuta vyanzo vipya vya uwekezaji.

### KUKIDHI MATAKWA YA KISHERIA

Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau wake. Lakini pia Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Madalali wa Soko la Hisa (Brokers) na benki za Biashara. Kwa mwaka 2021, Kampuni imeweza kutimiza taratibu na vigezo vyote kulingana na Matakwa ya Mamlaka husika.

### UPATIKANAJI WA TAARIFA YA MAHESABU

Kampuni ina wafanyakazi wenye uzoefu katika kitengo cha uhasibu na fedha. Vitabu vya mahesabu vimekuwa vikitunzwa na taarifa ya fedha inaandaliwa kulingana na Sheria ya Kimataifa ya Uandaaji wa taarifa za Mahesabu. (IFRS).

### MTAJI WA KAMPUNI

Mtaji wa Kampuni ulioidhinishwa ni Shilingi 100,000,000,000 ambapo umegawanywa katika mfumo wa hisa, ambapo kufikia Desemba 31, 2021 thamani ya hisa moja ilikuwa sawa na Shilingi 20. Hisa zilizokuwa zimelipiwa ni sawa na Shilingi 2,167,952.000

*Jedwali na. 10*

| | 2021<br>Shs'000 | 2020<br>Shs'000 |
|---|---|---|
| Mtaji wa Kampuni Ulioidhinishwa (Shs)<br>5,000,000,000 hisa za kawaida zenye thamani ya Shilingi 20 kwa hisa moja. | 100,000,000 | 100,000,000 |
| **Hiza zilizolipiwa**<br>72,957,660 hisa za kawaida zenye thamani ya Shilingi 20 kwa kila hisa. | 1,459,153 | 1,459,153 |
| Share Premium | 708,799 | 708,799 |
| | 2,167,952 | 2,167,952 |

**MTAJI WA KAMPUNI NA UMILIKI WAKE.**

*Jedwali na. 11*

| UMILIKI WA HISA | ASILIMIA | SHS'000 |
|---|---|---|
| PSSSF | 39 | 562,006 |
| Mkombozi Fishing & Marine Transport Ltd | 6 | 84,300 |
| Abbasi Export Ltd | 2 | 33,720 |
| Christopher Mwita Gachuma | 2 | 28,100 |
| Fayaz Feroz Rashid | 2 | 24,728 |
| Nimrod Elirehemah Mkono | 2 | 22,480 |
| Wanahisa wengine (less than 1.5) | 47 | 703,819 |
| | **100** | **1,459,153** |

**TAARIFA KUHUSU SOKO LA HISA**

Kampuni imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Mpaka kufikia Desemba 31, 2021, thamani ya hisa moja ilikuwa Shilingi 350 ambayo ni sawa na thamani ya hisa moja kwa mwaka 2020 na mtaji wa Soko ulikuwa Shilingi 25,580,000,000 ambayo ni sawa na mtaji wa mwaka 2020.

**BIASHARA ENDELEVU**

Katika majadiliano ya Bodi katika kuimarisha ukuaji wa Kampuni, haukuzingatia kushuka na kupanda kwa thamani ya fedha. Bodi ilizingatia kulinda na kuhakikisha Kampuni inaendeleza utendaji wake, mabadiliko ya tabia nchi na rasilimali zinazohitajika ili Kampuni iendelee kufanikiwa kwa miaka ijayo. Lakini pia tunaamini katika kuimarisha mazingira ya utendaji katika kuepuka kuwekeza kwenye miradi ambayo itaharibu sifa nzuri ya Kampuni hata kama utakuwa na faida kubwa; kuhimiza wafanyakazi na wadau wa Kampuni kujiendeleza, kujizoeza na kutumia teknolojia, kutumia mtandao, kuongeza upeo wa wafanyakazi wa TICL katika utendaji na kuwahimiza wadau wa Kampuni kuhusu kuondoa madhara ya kimfumo kupitia teknolojia. Kuelimisha kuhusu programu ya uhamasishaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira (Corporate Social Responsibilities).

## MTAZAMO KATIKA KUENDELEA KWA SHUGHULI ZA KAMPUNI

Wakurugenzi wanaamini kuwa, Kampuni ina rasilimali za kutosha za kifedha kuendelea kufanya kazi kwa siku zijazo kulingana na Taarifa ya Mahesabu iliyoambatanishwa. Wakurugenzi wamejiridhisha kuwa, Kampuni iko katika hali nzuri ya kifedha na kwamba ina uwezo wa kukopa ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha pale itakapohitajika. Wakurugenzi hawajapokea taarifa mpya ambayo inaweza kuathiri utendaji wa Kampuni hapo baadaye. Athari za Ugonjwa wa Corona (COVID – 19) zimezingatiwa katika utoaji wa taarifa hii.

## MASLAHI YA WAFANYAKAZI

Kampuni inawapa wafanyakazi wake maslahi yafuatayo:

### Elimu

Kampuni inawafadhili wafanyakazi wake kujiendeleza kielimu katika kozi za muda mfupi ndani na nje ya nchi kwa taaluma mbalimbali kulingana na uhitaji na kiwango cha fedha kinachohitajika. Kampuni pia inasaidia wafanyakazi pale wanapoamua kujiendeleza wenyewe kwa masomo ya muda mrefu.

### Mikopo kwa Wafanyakazi

Kampuni inatoa mikopo kwa wafanyakazi ya muda mrefu na mfupi kuweza kutatua matatizo ya kifedha na kufanya shughuli nyingine za kiuchumi za kujiongezea kipato. Mikopo hiyo inatolewa kulingana na masharti yaliyowekwa na Bodi na inatolewa kulingana na Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka husika.

### Msaada wa Kifedha

Kampuni inaandaa sera ya kusaidia pale mfanyakazi anapofariki au wategemezi.

### Mafao ya Kustaafu

Kampuni inachangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo Public Servant Social Security Fund (PSSSF) na National Social Security Fund (NSSF) kwa ajili ya mafao ya baadaye kwa wafanyakazi wake.

### Watu wasiojiweza (Walemavu wa Viungo)

Kampuni inatoa nafasi sawa ya ajira kwa watu wote yaani wenye viungo vyote na wale wenye ulemavu wa viungo.

### Huduma ya Matibabu

Kampuni imeingia mkataba na Shirika la Bima ya Afya la Taifa (NHIF) kutoa huduma ya afya kwa wafanyakazi wa Kampuni na wategemezi wao.

### Usawa wa Kijinsia Kazini

Kufikia Desemba 31, 2021, Kampuni ilikuwa na wafanyakazi 6 ukilinganisha na wanne mwaka 2020. Wafanyakazi watatu wakiwa ni wanawake na watatu wanaume ukilinganisha na mwaka 2020 ambapo wanaume walikuwa wawili na wanawake wawili.

### Mazingira, Jamii na Utawala

Tunaendelea kuzingatia masuala ya Mazingira, Kijamii na Utawala na tumetambua njia bora zaidi za kupima kile ambacho tumekuwa tukikifanya. Kampuni imejitolea "kuwa kijani" kwa kufanya kazi bila kutumia karatasi na kutenga uwekezaji wetu wa hisa katika makampuni ambayo yanatii sheria za mazingira na usalama.

## MIPANGO YA BAADAYE YA MAENDELEO

Kuanzia mwaka 2018, Bodi ya Wakurugenzi iliamua kupunguza uwekezaji wake kwenye hisa na kuwekeza maeneo mengine ambayo ilikuwa bado haijawekeza. Toka Kampuni imeanza kufanya shughuli za biashara Oktoba, 2005 zaidi ya asilimia tisini na tano (95%) ya uwekezaji wake ilikuwa ni kwenye hisa za makampuni yaliyoorodhesha hisa zake

kwenye Soko la Hisa. Bodi iliamua kuwekeza kwenye maeneo yenye mapato ya uhakika (Amana za Serikali, Amana za Makampuni na faida inayotokana na Amana za Mabenki). Bodi ya Wakurugenzi inaamini kwa kuwekeza katika taasisi hizi za kifedha ni biashara nzuri kwa kuzingatia pale ambapo Soko la Hisa litashindwa kufanya vizuri kama ilivyo sasa ambapo kipato chake hakitabiriki.

Bodi ya Wakurugenzi imeamua kuelekeza uwekezaji wake kwenye amana za serikali kwa sababu faida yake ni ya uhakika ukilinganisha na uwekezaji katika hisa.

Mwisho, Bodi inapenda kuainisha maeneo mengine ya uwekezaji kama kuagiza na kuuza bidhaa nje ya nchi, biashara ya mifugo, na biashara nyingine katika sekta ya fedha kama kuuza na kununua Amana za Makampuni na Serikali.

### Kulinda Mali za Kampuni
Wakurugenzi wana jukumu la kulinda mali za Kampuni. Bodi imeidhinisha sera mbalimbali na kanuni ambazo hazikinzani na Mamlaka za fedha, na sera ya uwekezaji ili kuimarisha mazingira ya udhibiti wa mfumo wa ndani. Sera hizi hupitiwa mara kwa mara ili kuenenda na mazingira ya sasa ya utendaji. Wakurugenzi wanayo furaha kutoa taarifa kwamba kwa mwaka 2021 hapakuwa na matukio yoyote ya udanganyifu.

### Mambo yahusuyo Miamala
Mambo yote yahusuyo miamala na kiwango cha fedha kilichopo kimeonyeshwa katika kifungu cha 32 cha Taarifa ya Fedha.

### Wajibu wa Wakurugenzi
Ni wajibu wa Wakurugenzi kuhakikisha kwamba taarifa za fedha zinawasilishwa kwa kila mwisho wa mwaka wa fedha na matokeo ya shughuli za utendaji kwa kipindi kilichomalizika, kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa taarifa za Fedha na taratibu zinazotumika, kanuni na matakwa ya kisheria. Wakurugenzi pia wanathibitisha matakwa ya Uandaaji wa Taarifa za Fedha Tanzania (TFRS 1) na sheria zingine zote zinazohusiana na Kampuni.

### WAKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI
Wakaguzi wa Mahesabu, Crowe Tanzania, wameendelea kuonyesha nia yao ya kuendelea kukagua mahesabu ya Kampuni endapo watateuliwa tena, kwa mwaka wa fedha utakaoishia tarehe 31 Desemba, 2022. Hata hivyo, Bodi itawasilisha pendekezo la uteuzi wa mkaguzi katika Mkutano huu kwa majadiliano na kuidhinisha.

Taarifa ya Mahesabu imeainishwa katika ukurasa wa 23 hadi 27, ambapo imeandaliwa vizuri na kuidhinishwa na Bodi katika Mkutano maalum uliofanyika tarehe 30/05/2022 na kusainiwa na wajumbe wafuatao:

| | |
|---|---|
| ........................................................ | ........................................................ |
| Bwn. Fortunatus M. Magambo | Pro. Lucian Msambichaka |
| **Mkurugenzi** | **Mkurugenzi** |
| Tarehe:**30/05/2022** | Tarehe:**30/05/2022** |

# UTHIBITISHO WA MKUU WA IDARA YA UHASIBU

Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA) kulingana na uwezo wake katika kuwapima na kusajili Wahasibu na wakaguzi wa mahesabu pamoja na sheria ya makampuni namba thelathini na tatu (33) ya mwaka 1972, na kurekebishwa na sheria namba mbili (2) ya mwaka 1995, inaitaka Taarifa ya mahesabu kuambatanishwa na uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha/ Mahesabu aliyehusika kuandaa taarifa ya Fedha ya Kampuni husika. Mtaalam wa Mahesabu anapaswa kuwasaidia Wakurugenzi/ Wafanyakazi kutekeleza jukumu la kuandaa taarifa za kifedha za taasisi inayotoa picha halisi ya Kampuni na utendaji wake kulingana na Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa na matakwa ya kisheria ya uandaaji wa taarifa za kifedha. Jukumu kamili la kisheria kwa utayarishaji wa taarifa za kifedha liko kwa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoonyeshwa hapo juu kwenye Wajibu wa Wakurugenzi.

Mimi Joel Chikoma, nikiwa ni Mkuu wa idara ya Uhasibu ya TCCIA INVESTMENT PLC ninathibitisha kwamba, Taarifa ya Mahesabu ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021 imeandaliwa kulingana na viwango vya Uhasibu na matakwa ya Kisheria. Ninathibitisha kwamba, Taarifa ya Mahesabu inatoa picha kamili ya TCCIA INVESTMENT PLC kufikia tarehe hiyo iliyotajwa hapo juu na kwamba zimeandaliwa kulingana na taarifa za kifedha zinazotunzwa vizuri.



**Joel Chikoma**
Mkuu wa Idara ya Uhasibu na Uwekezaji
NBAA Membership No: ACPA 3285
Tarehe:**30/05/2022**

# MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2021

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2021

| | 2021 Shilingi '000 | 2020 Shilingi '000 |
|---|---|---|
| Mapato | 2,690,726 | 2,507,571 |
| Mapato anuwai | 200,183 | 13,360 |
| Mapato mengine/ (hasara) ya uendeshaji | **36,952** | (1,347,870) |
| Matumizi ya uendeshaji | (1,014,150) | (1,060,243) |
| **Faida ya uendeshaji** | **1,913,711** | **112,818** |
| Gharama za mtaji | (374,670) | (466,557) |
| **Faida/ (hasara) kabla ya kodi** | **1,539,041** | **(353,739)** |
| Kodi | (209,182) | (121,397) |
| **Faida/(Hasara) kwa mwaka** | **1,329,859** | **(475,136)** |
| **Mapato mengine kamili** | | |
| Kupanda/ (kushuka) kwa thamani ya hisa | (58,088) | 388,225 |
| **Mapato/(hasara) mengine ya mwaka** | **(58,088)** | **388,225** |
| **Jumla ya mapato/(hasara) kwa mwaka** | **1,271,771** | **(86,911)** |
| **Mapato kwa kila hisa** | **18.22** | **(6.51)** |

## TAARIFA YA WARAKA WA MIZANIA HADI TAREHE 31/12/2021

| Rasilimali | 2021<br>Shilingi' 000 | 2020<br>Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali za muda mrefu** | | |
| Mali ya kudumu inayogusika | 139,447 | 26,307 |
| Haki ya matumizi ya rasilimali | 3,256 | 42,316 |
| Uwekezaji wa kwenye ardhi/majengo | 221,347 | 221,347 |
| Uwekezaji wa kwenye hisa | 15,253,840 | 14,848,114 |
| Dhamana za serikali | 12,985,104 | 13,578,175 |
| Rasilimali zisizogusika | 4,500 | - |
| Amana za makampuni/mashirika | - | - |
| Uwekezaji mwingine | - | - |
| | **28,607,494** | **28,716,259** |
| **Rasilimali za muda mfupi** | | |
| Rasilimali za biashara | 589,870 | 571,177 |
| Kodi ya muda mfupi | 242,682 | 273,350 |
| Amana za makampuni/mashirika | - | 10,000 |
| Fedha na thamani ya fedha | 1,011,299 | 206,233 |
| | **1,843,851** | **1,060,76** |
| **Jumla ya Rasimali** | **30,451,345** | **29,777,019** |
| **Mtaji na Madeni** | | |
| **Mtaji** | | |
| **Mtaji** | 2,167,952 | 2,167,952 |
| Jumla ya akiba | 5,327,762 | 5,430,850 |
| Faida kuu | 19,908,600 | 18,972,207 |
| | **27,404,314** | **26,571,009** |
| **Madeni ya muda mrefu** | | |
| Mkopo wa muda mrefu | 2,396,962 | 2,606,193 |
| Kodi iliyoahirishwa | 23,890 | 3,256 |
| | **2,420,852** | **2,609,449** |

| Rasilimali | 2021<br>Shilingi' 000 | 2020<br>Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Madeni ya muda mfupi** | | |
| Madeni ya biashara | 132,095 | 151,075 |
| Dhima ya kukodisha | - | 39,093 |
| Mkopo wa muda mfupi | 209,231 | 183,092 |
| Gawio | 284,853 | 223,301 |
| | **626,179** | **596,561** |
| **Jumla ya madeni** | **3,047,031** | **3,206,010** |
| **Jumla ya mtaji na madeni** | **30,451,345** | **29,777,019** |

**TAARIFA YA WARAKA WA MIZANIA HADI TAREHE 31/12/2021**

Taarifa hii ya mahesabu ilithibitishwa kwa ajili ya kutangazwa na Bodi na ilisainiwa kwa niaba yao na:

..........................................................

Bwn. Fortunatus M. Magambo
**Mkurugenzi**
Tarehe:**30/05/2022**

..........................................................

Pro. Lucian Msambichaka
**Mkurugenzi**
Tarehe:**30/05/2022**

# TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA 2021

| | Mtaji wa hisa | Mapato ya hisa | Jumla ya mtaji wa hisa | Akiba ya thamani ya uwekezaji kwenye hisa | Gharama ya IPO | Faida kuu | Jumla ya mtaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shilingi '000 | '000 | '000 | '000 | '000 | '000 | '000 |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 01/01/2020** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **9,650,287** | **(629,662)** | 15,907,807 | **27,096,384** |
| **Hasara ya mwaka** | | | | | | (475,136) | (475,136) |
| **Mapato mengine** | | | | 388,225 | - | - | 388,225 |
| **Kuhamisha kwenda akiba kuu** | | | | (3,978,000) | | 3,978,000 | - |
| **Gawio** | | | | | | (438,464) | (438,464) |
| **Usawa tarehe 31/12/2020** | 1,459,153 | 708,799 | 2,167,952 | 6,060,512 | (629,662) | 18,972,207 | 26,571,007 |
| **Muda wa sasa:** | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 01/01/2021** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **9,650,287** | **(629,662)** | **18,972,207** | **26,571,007** |
| **Mapato ya mwaka** | | | | | | 1,329,859 | 1,329,859 |
| **Mapato mengine** | | | | (58,088) | | | (58,088) |
| **Kuhamisha** | | | | | | | |
| **kwenda akiba kuu** | | | | (45,000) | | 45,000 | |
| **Gawio** | | | | | | (438,464) | (438,464) |
| **Usawa tarehe** | | | | | | | |
| **31/12/2021** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **5,957,424** | **(629,662)** | **19,908,602** | **27,404,314** |

# TAARIFA YA MZUNGUKO WA FEDHA

| | 2021 | 2020 |
|---|---|---|
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uendeshaji** | **Shilingi '000** | **Shilingi '000** |
| Fedha iliyotoka kwenye shughuli za uendeshaji | 1,908,698 | 1,461,036 |
| Gharama za kifedha | (374,670) | (466,557) |
| Kadi iliyolipwa | (157,880) | (49,835) |
| **Fedha taslimu inayotokana na uendeshaji** | **1,376,148** | **944,644** |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uwekezaji** | | |
| Manunuzi ya mali ya kudumu inayogusika | (142,192) | (11,600) |
| Manunuzi ya Haki ya kutumia Rasilimali | - | (74,866) |
| Manunuzi ya Rasilimali Isiyogusika | (6,000) | - |
| Mzunguko kwenye uwekezaji katika hisa | (463,814) | 4,904,999 |
| Manunuzi ya amana za serikali | 593,071 | (3,900,253) |
| Mzunguko kwenye amana za makampuni | 10,000 | 20,336 |
| Faida/(Hasara) kwenye uuzaji wa hisa | 36,952 | (1,342,370) |
| **Fedha taslimu iliyotumika katika uwekezaji** | **28,017** | **(403,754)** |
| Mzunguko wa mkopo | (183,094) | (210,715) |
| Mzunguko wa dhima ya kukodisha | (39,093) | 39,093 |
| Gawio lililolipwa | (376,912) | (387,349) |
| **Fedha taslimu iliyotokana na mtaji** | **(599,099)** | **(558,971)** |
| **Jumla ya fedha taslimu za mzunguko kwa mwaka** | **805,066** | **(18,081)** |
| Fedha na thamani ya fedha mwanzo wa mwaka | **206,233** | 224,314 |
| **Fedha na thamani ya fedha mwisho wa mwaka** | **1,011,299** | **206,233** |

Dondoo Na. 17/5/2022

## WASILISHO

**WASILISHO:**

Ndugu Wanahisa mnaombwa kupokea na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021 na kuazimia kama ifuatavyo.

# "Azimio la 2/2022

Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021 imepitishwa kama ilivyowasilishwa."



# KUTANGAZA GAWIO

## KUTANGAZA GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioshia Desemba, 31 2021, Bodi inapendekeza kulipa gawio la shilingi 10 kwa hisa (2020: shilingi 6 kwa hisa).

## WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

## Azimio la 3/2022

"Mkutano Mkuu umeazimia, kuridhia pendekezo hili kwamba gawio la shilingi za Kitanzania Kumi (10) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi."



## UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2022


Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2021, Mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya CROWE Tanzania. Hadi sasa Bodi imeridhika na kazi ambayo ilifanywa na Kampuni hii kwa mwaka 2021. Aidha Kampuni hiyo imeonyesha nia ya kuendelea kukagua Mahesabu ya Kampuni yetu kama watateuliwa tena.

### WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2022. Ada ya ukaguzi inayopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 20 milioni Kabla ya kodi. Ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

## Azimio la 4/2022

"Imeazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Desemba 31, 2022. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 20 milioni kabla ya kodi kama gharama za malipo ya ukaguzi wa Mahesabu ya Kampuni."



## PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting".

Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi. Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

### WASILISHO

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha utakaoishia Desemba 31, 2022, Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000). Kama ilivyokuwa mwaka jana.

## Azimio la 5/2022

"Imeazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi."



Dondoo Na. 17/9/2022

## KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA PENDEKEZO LA KAMPUNI KUNUNUA BAADHI YA HISA ZAKE (SHARE BUY BACK)

Kwa miaka kadhaa Menejimenti imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wanahisa ambao wanahitaji kuuza hisa zao, lakini wakashindwa kutokana na kukosekana kwa wanunuzi. Taarifa za Soko la Hisa za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kulikuwa na hisa 140,000 ambazo hazijanunuliwa.

**Mapendekezo**

Bodi inapendekeza kuwa, Kampuni itenge shilingi milioni mia moja kwa kila mwaka mfulilizo kwa miaka mitatu kulingana na bei ya soko. Lengo la kuandaa Mfumo huu wa Kampuni kununua hisa zake, ni kutokana na sababu zifuatazo;

- Mfumo huu utaiwezesha Kampuni kuwarudishia wanahisa wake fedha zao kulingana na umiliki wao, na hivyo kuhamasisha wanahisa kuzinunua tena hapo baaadae.
- Mfumo huu utasaidia kuboresha mapato katika uwekezaji na kuongeza thamani ya hisa katika soko.
- Kampuni inaamini kuwa mchakato huu ambao pia unahusisha wanahisa wadogo utawanufaisha wanahisa wengi, ambao mara nyingi wameshindwa kuuza hisa zao kwa sababu ya changamoto ya kutopata wanunuzi katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).
- Hisa zitakazonunuliwa na Kampuni zinaweza kuuzwa tena katika siku zijazo pale wanunuzi wengine watakapojitokeza.
- Hisa zitakazonunuliwa na Kampuni hazitakuwa na gawio, hivyo kusaidia kuongezeka kwa thamani ya hisa.

**Wasilisho**

Pendekezo hili linawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu ili Kujadiliwa na Kuidhinishwa.

**Bodi ya Wakurugenzi.**

## Azimio la 6/2022

"Imeazimiwa kwamba Kampuni kununua baadhi ya Hisa zake kama ilivyopendekezwa na bodi ya Wakurugenzi"

Dondoo Na. 17/10/2022

## PENDEKEZO LA KUORODHESHA HISA ZA KAMPUNI KWENYE SOKO LA HISA LA AFRINEX- MAURITIUS (CROSS-LISTING)

Bodi inapenda kuchukua fursa hii kuwasilisha mbele ya Mkutano Mkuu pendekezo la kuorodhesha, Kampuni yetu kwenye soko la Kimataifa la Dhamana na Mitaji AFRINEX nchini Mauritius (Cross listing) amabalo ni lango la kupanua wigo wa kukutanisha watoa Mitaji wa Africa na Duniani kote. Sababu ya kuleta pendekezo la kuorodhesha Kampuni kwenye soko la Kimataifa ni;

- Kupanua vyanzo vya kuongeza mtaji kwa ajili ya kupanua wigo wa uwekezaji. Mpaka sasa tumekuwa tunategemea fedha za wakezaji wa hapa Nchini.
- Kuwawezesha Wanahisa ambao wanahitaji kuuza hisa zao kupata wanunuzi wa nje.
- Ni soko pekee linalotoa huduma za kifedha (Pan-African Exchange) kwa watoa huduma wa Afrika na Wawekezaji wa Kimataifa.
- Kutoa fursa kwa wawekezaji wa Kimataifa ambao wanataka kuwekeza kwenye Kampuni yetu.
- Kuipa Kampuni fursa ya kujulikana na kuongeza muonekano kimataifa na kuvutia Wawekezaji na Taasisi zinazohitaji kuwekeza Tanzania kwa kushirikiana na Makampuni ya kizalendo ambayo yanatambulika kimataifa.
- Kuwezesha kampuni kupata fedha kwa kutoa hati fungani na kushiriki kwenye miradi mikubwa ya kimkakati kwani ni rahisi kukusanya fedha kwa aina zote za watoaji mitaji katika wigo mpana.
- Kanuni za wazi za kuorodhesha na za kiwango cha Kimataifa.

**Wasilisho**

Kuridhia Pendekezo la kuorodhesha hisa za Kampuni baada ya kukamilisha hatua zinazotakiwa kwenye Soko la Hisa la Kimataifa Mauritius.

Kurekebisha maeneo ya Katiba ambayo yataonekana yanahitaji kufanyiwa marekebisho ili kukidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Mamlaka husika.

## Azimio la 7/2022

"Imeazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa Kampuni kuorodhesha hisa zake kwenye soko la Hisa AFRINEX- MAURITIUS (CROSS-LISTING)"

## MAJINA YA WANAHISA PAMOJA NA WAWAKILISHI WA WANAHISA WALIODHURIA MKUTANO MKUU WA 16


Kiambatisho no.1

| SNO | CDS | JINA LA MWANAHISA | HISA | WALIOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 585373 | PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND 585373TCCIA001 | 28,100,300 | Mwakilishi |
| 2 | 569364 | MKOMBOZI FISHING & MARING TRANSPORT LTD 569364TCCIA001 | 4,215,000 | Mwakilishi |
| 3 | 569351 | ABBASI EXPORTS LTD 569351TCCIA001 | 1,686,000 | Mwakilishi |
| 4 | 150344 | CHRISTOPHER MWITA GACHUMA 150344TCCIA001 | 1,405,000 | Mwakilishi |
| 5 | 121481 | FAYAZ FEROZ RASHID 121481TCCIA001 | 1,236,400 | Mwanahisa |
| 6 | 46802 | NIMROD ELIREHEEMAH MKONO 46802TCCIA001 | 1,123,975 | Mwakilishi |
| 7 | 149308 | ZUMBI ELVIS MUSIBA(ADMIN) ELVIS ARISTABLUS MUSIBA(DECEASED) 149308TCCIA001 | 674,375 | Mwanahisa |
| 8 | 569116 | JAMES MAJUKANO GEGE 569116TCCIA001 | 561,975 | Mwakilishi |
| 9 | 105271 | LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA 105271TCCIA001 | 464,200 | Mwanahisa |
| 10 | 569310 | JULIUS MATIKO MWITA 569310TCCIA001 | 323,150 | Mwanahisa |
| 11 | 569170 | JANE ROBERT MASABARI 569170TCCIA001 | 281,000 | Mwanahisa |
| 12 | 55965 | ZAHIR WAZIRI LEYSUYAH 55965TCCIA001 | 210,737 | Mwanahisa |
| 13 | 100793 | ELISANTE ELIKANA MURO 100793TCCIA001 | 140,500 | Mwanahisa |
| 14 | 124080 | MAGDALENA NELSON ENOCK MKOCHA 124080TCCIA001 | 102,362 | Mwanahisa |
| 15 | 569106 | ASUNGWILE BASALILE MWANGUNGULU 569106TCCIA001 | 70,250 | Mwanahisa |
| 16 | 569533 | DISMAS MORRIS MOKUNDA 569533TCCIA001 | 70,250 | Mwanahisa |
| 17 | 119924 | ZELDA MUTAGAHYWA BARUTI (ADMIN) ELIAS EMMANUEL BARUTI(DECEASED) 119924TCCIA001 | 70,250 | Mwanahisa |
| 18 | 569748 | TAMIM WALIJI AMIJEE 569748TCCIA001 | 56,200 | Mwanahisa |
| 19 | 569279 | DR.VICENT ISAAC MHADA 569279TCCIA001 | 56,200 | Mwakilishi |
| 20 | 569240 | ABERHARD JOHN MBEPERA 569240TCCIA001 | 56,200 | Mwanahisa |
| 21 | 569333 | TCCIA MOROGORO 569333TCCIA001 | 56,200 | Mwanahisa |
| 22 | 569251 | MSANGI MABIRANGA TSETONGA 569251TCCIA001 | 56,200 | Mwanahisa |
| 23 | 569907 | MOHAMED BURHAN 569907TCCIA001 | 56,200 | Mwanahisa |
| 24 | 107183 | MOHAMEDRAFIK AKBER PARPIA 107183TCCIA001 | 56,200 | Mwakilishi |
| 25 | 569222 | JACKSON ZEPHANIA LUDIGIJA 569222TCCIA001 | 56,200 | Mwanahisa |
| 26 | 145139 | FARZANA SALIM KHAKOO 145139TCCIA001 | 37,000 | Mwanahisa |
| 27 | 569334 | TCCIA MTWARA 569334TCCIA001 | 28,100 | Mwanahisa |
| 28 | 569965 | SEBASTIAN JOSEPH KUNJUMU 569965TCCIA001 | 28,100 | Mwanahisa |
| 29 | 569952 | JOHN ROTENTE CHACHA 569952TCCIA001 | 28,100 | Mwanahisa |
| 30 | 569934 | BONIFACE DONALD MAKERE 569934TCCIA001 | 28,100 | Mwakilishi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 31 | 588472 | JANE LAMECK CHACHA 588472TCCIA001 | 28,088 | Mwanahisa |
| 32 | 148116 | STELLA MARO HIRJI 148116TCCIA001 | 21,050 | Mwanahisa |
| 33 | 569827 | THOMAS RUGUMBA GHATI 569827TCCIA001 | 19,813 | Mwanahisa |
| 34 | 222028 | NATHAN EDWARD MNYAWAMI 222028TCCIA001 | 19,675 | Mwanahisa |
| 35 | 569559 | JULIUS MUTABUZI KAIJAGE 569559TCCIA001 | 16,863 | Mwanahisa |
| 36 | 569161 | KANYENYE KISULILA MATANGA 569161TCCIA001 | 16,863 | Mwanahisa |
| 37 | 220656 | TCCIA 220656TCCIA001 | 15,000 | Mwanahisa |
| 38 | 569184 | JOEL TIMOTH CHIKOMA 569184TCCIA001 | 14,613 | Mwanahisa |
| 39 | 569442 | JULIUS MARWA MACHAGE 569442TCCIA001 | 14,050 | Mwanahisa |
| 40 | 570005 | ALEXANDER ITAMBE MASSAY 570005TCCIA001 | 14,050 | Mwanahisa |
| 41 | 570052 | ZENA HASHIM HASSAN 570052TCCIA001 | 14,050 | Mwanahisa |
| 42 | 228299 | ISARIA KAWEDI MWENDE 228299TCCIA001 | 12,500 | Mwanahisa |
| 43 | 569180 | GRACEANA BAKARI KILENGA 569180TCCIA001 | 11,238 | Mwanahisa |
| 44 | 569806 | THERESIA PETER UMBU DUKA LA REJAREJA 569806TCCIA001 | 11,237 | Mwanahisa |
| 45 | 38047 | EMMANUEL JOSEPH DAFTARI 38047TCCIA001 | 10,000 | Mwanahisa |
| 46 | 132074 | SAMWEL FREDERICK MANDARA 132074TCCIA001 | 10,000 | Mwanahisa |
| 47 | 546551 | JUBILATE BERNARD MINJA 546551TCCIA001 | 10,000 | Mwanahisa |
| 48 | 569168 | KENNEDY NELSON SIMUNDI 569168TCCIA001 | 9,985 | Mwanahisa |
| 49 | 570113 | SAMO ELIAS MWITA 570113TCCIA001 | 8,425 | Mwanahisa |
| 50 | 569211 | MAYASSA MOHAMED SHARIF MUBAGO 569211TCCIA001 | 7,025 | Mwanahisa |
| 51 | 71772 | MICHAEL THOMAS KWEKA 71772TCCIA001 | 5,625 | Mwanahisa |
| 52 | 569372 | KAMTECH ENTERPRISES 569372TCCIA001 | 5,625 | Mwanahisa |
| 53 | 132662 | CALVERT MAZEYNZILE NKURLU 132662TCCIA001 | 5,625 | Mwanahisa |
| 54 | 569803 | ISHMAEL SAGIRAKI LAISER 569803TCCIA001 | 5,625 | Mwanahisa |
| 55 | 569206 | DR.TUMAINI EDWARD MHADA 569206TCCIA001 | 5,625 | Mwakilishi |
| 56 | 169700 | EMMANUEL VITALIS MUSHI 169700TCCIA001 | 5,625 | Mwanahisa |
| 57 | 134364 | STEPHEN MASANJA MWILOLEZI 134364TCCIA001 | 5,625 | Mwanahisa |
| 58 | 569661 | SWEETBERT RUMANYIKA MUSHOBOZI 569661TCCIA001 | 5,625 | Mwanahisa |
| 59 | 88062 | SYNPHOROSE EVARIST BAITWA 88062TCCIA001 | 5,000 | Mwanahisa |
| 60 | 546494 | WYLIFFE PETER MAKONGORO 546494TCCIA001 | 5,000 | Mwanahisa |
| 61 | 504917 | ISRAEL EMMANUEL KINGU 504917TCCIA001 | 5,000 | Mwanahisa |
| 62 | 526870 | JOHN MARTIN LYANGA 526870TCCIA001 | 5,000 | Mwanahisa |
| 63 | 569411 | MENAS MARKO LIKUKU 569411TCCIA001 | 4,775 | Mwanahisa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 64 | 124405 | REBECCA OBASSI KATULE 124405TCCIA001 | 3,000 | Mwanahisa |
| 65 | 569831 | HILDAGARDA CUTHBERT NTAMUTURAMO 569831TCCIA001 | 2,813 | Mwanahisa |
| 66 | 569752 | JULIUS MATIKU MWEMBEI 569752TCCIA001 | 2,813 | Mwanahisa |
| 67 | 569316 | CHAWATA (M) TABORA 569316TCCIA001 | 2,813 | Mwanahisa |
| 68 | 153300 | DOREEN SEMALI KISAMO 153300TCCIA001 | 2,813 | Mwanahisa |
| 69 | 570465 | DOMINIC LUSASI 570465TCCIA001 | 2,813 | Mwanahisa |
| 70 | 569632 | STEVEN SABHI MWITA 569632TCCIA001 | 2,812 | Mwanahisa |
| 71 | 569732 | AGNESS ROBERT LIMBU 569732TCCIA001 | 2,812 | Mwanahisa |
| 72 | 569700 | ZAIDIA AHMADA KANTANGAYO 569700TCCIA001 | 2,812 | Mwanahisa |
| 73 | 569215 | ZUHURA MOHAMED MUBAGO 569215TCCIA001 | 2,812 | Mwanahisa |
| 74 | 569303 | BENEDICT MPEJIWA MASSELE 569303TCCIA001 | 2,812 | Mwanahisa |
| 75 | 570601 | MAIMUNA SALUM NAMKUMBE 570601TCCIA001 | 2,812 | Mwanahisa |
| 76 | 184221 | ROGERS MOSES HINJU 184221TCCIA001 | 2,812 | Mwanahisa |
| 77 | 150494 | RAPHAEL  MWITA AKIRI 150494TCCIA001 | 2,500 | Mwanahisa |
| 78 | 546511 | PRAYGOD ANDREW MBAGA 546511TCCIA001 | 2,500 | Mwanahisa |
| 79 | 514470 | MWANJAA SAID LYEZIA 514470TCCIA001 | 2,500 | Mwanahisa |
| 80 | 395039 | BARNABAS O MAFURU 395039TCCIA001 | 2,500 | Mwanahisa |
| 81 | 505800 | DEOGRATIUS ANDREW CHUWA 505800TCCIA001 | 2,500 | Mwanahisa |
| 82 | 517133 | SHUKURU ABASS NASSOR 517133TCCIA001 | 2,000 | Mwanahisa |
| 83 | 569491 | DORAH LEO MTWEVE 569491TCCIA001 | 1,688 | Mwanahisa |
| 84 | 437763 | MJAHIDI B KAMUGISHA 437763TCCIA001 | 1,500 | Mwanahisa |
| 85 | 569262 | CYPRIAN GEOFREY MWELLAH 569262TCCIA001 | 1,400 | Mwanahisa |
| 86 | 569187 | JOHN OLENANGASON MOLLEL 569187TCCIA001 | 1,400 | Mwanahisa |
| 87 | 570856 | EUGENIA ALOYCE YOMBA 570856TCCIA001 | 1,400 | Mwanahisa |
| 88 | 569669 | HARUNA ABASS IBELLA 569669TCCIA001 | 1,400 | Mwanahisa |
| 89 | 569146 | DOMINIC DANIEL KYARUZI 569146TCCIA001 | 1,400 | Mwanahisa |
| 90 | 571100 | ZUHULA MFAUME SELEMANI 571100TCCIA001 | 1,400 | Mwanahisa |
| 91 | 168565 | VITALIS KULINDWA SHIJA 168565TCCIA001 | 1,400 | Mwanahisa |
| 92 | 513922 | ELIYA NGUVU YA BWANA DAUDI 513922TCCIA001 | 1,250 | Mwanahisa |
| 93 | 546380 | ESHI EMMANUEL  MBISE 546380TCCIA001 | 1,000 | Mwanahisa |
| 94 | 253930 | ALOYCE SANULA SWILA 253930TCCIA001 | 1,000 | Mwanahisa |
| 95 | 546521 | BENJAMIN BWIRE  KISAKI 546521TCCIA001 | 1,000 | Mwanahisa |
| 96 | 145499 | KELVIN MATHIAS MASUNGA MASENDE 145499TCCIA001 | 1,000 | Mwanahisa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 97 | 253152 | AMBROSE REMMY MWAKIMBWALA 253152TCCIA001 | 750 | Mwanahisa |
| 98 | 522833 | HASHIM SAID OMARY 522833TCCIA001 | 500 | Mwanahisa |
| 99 | 546253 | ISSA JUMA ISSA 546253TCCIA001 | 500 | Mwanahisa |
| 100 | 546422 | REVOCATUS BELLE RUMISHA 546422TCCIA001 | 500 | Mwanahisa |
| 101 | 546327 | FRANCO JOHN MBEGALLO 546327TCCIA001 | 300 | Mwanahisa |
| 102 | 585985 | PETER WILLIAM KIFUNGUOMALI 585985TCCIA001 | 270 | Mwanahisa |
| 103 | 527294 | PROSPER JOHN ASSENGA 527294TCCIA001 | 250 | Mwanahisa |
| 104 | 264248 | DANIEL WILSON CHARO 264248TCCIA001 | 250 | Mwanahisa |
| 105 | 546801 | DEOGRATIAS ATHANAS MROSSO 546801TCCIA001 | 200 | Mwanahisa |
| 106 | 545998 | MKAYALA SIMBA KALINDULAH 545998TCCIA001 | 200 | Mwanahisa |
| 107 | 546560 | MAANYA MOHAMED SOLISI 546560TCCIA001 | 200 | Mwanahisa |
| 108 | 553205 | HELLEN RAPAHEL LAIZER ITF JULIETH CHRISTOPHER MUSHENDWA 553205TCCIA001 | 200 | Mwanahisa |
| 109 | 546604 | NEDUVOTO PINIEL MOLLEL 546604TCCIA001 | 200 | Mwanahisa |
| 110 | 544562 | THOMAS TUNIGA JACOB 544562TCCIA001 | 200 | Mwanahisa |
| 111 | 546920 | VERONICA STEPHANO MARWA 546920TCCIA001 | 120 | Mwanahisa |
| 112 | 543201 | PIUS KUSEKWA ELIAS 543201TCCIA001 | 120 | Mwanahisa |
| 113 | 546446 | PETER JOHN LISUNGU 546446TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 114 | 546235 | NICKO MWADUPA HENRY 546235TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 115 | 546703 | HUMPHREY PHILIP PALALLO 546703TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 116 | 546602 | MANASE LOILANGWAKI MBESERE 546602TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 117 | 546252 | JUSTINE NGOKA FUE 546252TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 118 | 545126 | ZAKAYO MICHAEL MKALI 545126TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 119 | 546505 | GEOFFREY ROBERT NYANGUSI 546505TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 120 | 546526 | EDGAR NGOMBALE 546526TCCIA001 | 100 | Mwanahisa |
| 121 | 152601 | MONICA HAULE MWASALYANDA 152601TCCIA001 | 1 | Mwanahisa |
| | | | **41,764,072** | |



# KUFUNGA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA

**TCCIA INVESTMENT PLC**
P.O.Box 72678 Dar es Salaam, Tanzania
Tel: 255 – 22 – 276 0172/27601725
Fax: 255 – 22 – 2119437
Email: info@tcciainvest.co.tz,
Web site: http://www.tcciainvest.co.tz